

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA THELATHINI NA MOJA

18 JUNI, 2015



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA THELATHINI NA MOJA – TAREHE 18 JUNI, 2015

I. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU

219. MHESHIMIWA MOSES JOSEPH MACHALI (KASULU MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-
Mnamo mwaka 2011 na Desemba, 2013 kwa nyakati tofauti Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi kumaliza tatizo la Wakulima wa Kasulu wanaolima katika eneo la Kagera Nkanda wanaofukuzwa na kupigwa kila mwaka kwa agizo la Mkuu wa Wilaya ya Kasulu:-

Je, ni sababu gani zinazokwamisha kushughulikiwa kwa suala hilo kwa takribani miaka mitano sasa.

220. MHESHIMIWA ALIKO NIKUSUMA KIBONA (ILEJE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Wanafunzi wengi wa Shule za Kata na za Wananchi wamekuwa wakifanya vibaya katika masomo ya Sayansi kwa shule hizo kukosa vifaa vya kufundishia masomo hayo; na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imepandisha sifa za kujiunga na mafunzo ya Kada ya Afya kwa kumtaka mhitimu kuwa na *credit* katika masomo ya Sayansi:-

- (a) Je, kwa kufanya hivyo Serikali haioni ni kutengeneza ufa na ubaguzi kwa wenye nacho kuendelea kuwa nacho na wasio nacho kuendelea kuwa watawaliwa;
- (b) Je, Serikali haioni ipo haja ya kurejea kwenye misingi ya Azimio la Arusha ya kila mtu kupata haki sawa bila kubaguliwa kwa sababu ya kipato ili kuendelea kulinda umoja, upendo na mshikamano katika Taifa.

WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:

221. MHESHIMIWA MCH. ISRAEL YOHANA NATSE (KARATU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika:- SACCOS ni chombo kilichoundwa kwa lengo la kuleta ukombozi wa kiuchumi kwa watu wa hali ya chini lakini inasikitisha kuona kuwa SACCOS hizo hazikidhi malengo yake ya kuwanufaisha wanachama wake kwa sababu mbalimbali kama vile, ubadhilifu wa fedha, Vitendo vinavyofanywa na Viongozi wa SACCOS hizo, ilihali kuna Maafisa Ushirika wanaopaswa kudhibiti hali hiyo; Ushiriki wa Viongozi wa Kisiasa unaosababisha zifanye vibaya na mfano mzuri ni SACCOS za Halmashauari ya Karatu za Ayalabe, Mbulumbulu na Karatu SACCOS ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania:-

- (a) Je, ni nini nafasi ya Afisa Ushirika kama jicho la Serikali katika kuhakikisha kuwa SACCOS zinatimiza malengo yake;
- (b) Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu ushiriki wa Viongozi wa Kisiasa kwenye SACCOS ambao umekuwa ni tatizo kubwa.

WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

222. MHESHIMIWA RITTA ENESHER KABATI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Mikoja ya Iringa na Njombe inafahamika kwa kuwepo kwa hazina kubwa ya rasilimali ya madini ya chuma, hususan eneo la Liganga Wilayani Ludewa:-

Je, Serikali imefikia wapi katika Mkakati wa kuvuna rasilimali hii ya chuma ili kuendeleza viwanda vya chuma nchini na kuleta mabadiliko ya viwanda nchini.

WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:

223. MHESHIMIWA RIZIKI OMAR JUMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto:- Katika Mwaka wa Fedha 2012/2014 serikali ilitenga Tshs. Bilioni Mbili (2,000,000,000/=) kwa ajili ya mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na atika kipindi cha Julai – Desemba, 2013 Wizara ilipokea kiasi cha Tshs. 515, 628,846/= tu kutoka Wizara ya Fedha:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kuwa fedha hiyo inapatikana ili kuwaendeleza wanawake kiuchumi;

(b) Je, ni mikoa mingapi hadi sasa imefaidika na mfuko huo.

II. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

Muswada wa Sheria ya Masoko ya Bidhaa wa Mwaka 2015 (*The Commodity Exchanges Bill, 2015*);

Muswada wa Sheria ya Kuwalinda watoa taarifa za Uhalifu na Mashahidi wa Mwaka 2015 (*The Whistleblower and witness Protection Bill, 2015*)

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)

Kwamba, Bunge likubali kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2014 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

WAZIRI WA FEDHA:

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha, 2015/2016.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
18 JUNI, 2015**

**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**

